

Hii gazeti ina andikwa na shirika lisilokuwa la kiserekali Internews kwa ushirikiano na wizara ya afia na Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekunda na Jumuiya Nyekunda kwa kujibu kwenyi mahitaji za habari ya jamii.

Kila juma, tunakusanya na kuchambua maoni ya jamii (uvumi yani habari zenye hazina uhakika, wasiwasi, maulizo, na kazalika) na tunatafuta majibu ku toka kwa wataalamu kwa kushirikisha jamii. Maulizo hizo zinachunguzwa kulingana na maana (umuhimu) yazo na mwendeleo wazo.


Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio "Koma Ebola"

[soundcloud.com/user-740750674](https://soundcloud.com/user-740750674)

[Facebook.com/komaebola](https://facebook.com/komaebola)

[@Ebolakoma](https://twitter.com/Ebolakoma)

[koma-ebola.info](https://koma-ebola.info)



## EBOLA

### SWALI

Gisi balifunga vituo vyote vya matunzo ya Ebola, kama kesi zingine zinajitokeza, tutaweka wagonjwa wapi?

### JIBU

Vituo vyote vya matunzo ya Ebola (CTE) havifungiwe kwa mara moja. Kufungiwa inafanyika moja kwa moja na inafuatana na hali ya hatari ya kila eneo ya afya. Kila kesi yenye inajitokeza na kuhakikishwa, itatunziwa ndani ya vituo vya matunzo ya Ebola vyenye vingali vinatumika. Uchaguzi ya kituo cha matunzo itafanyika kufuatana na gisi kinakaribia kwenye kesi hiyo inatangazwa.

Kisha kutangazwa mwisho wa muripuko ya magonjwa, vituo vyote vya matunzo ya Ebola vitafungwa.

Kujitokeza kwa kesi mpya kisha utangazaji itakuwa muripuko mpya ya magonjwa na kwa hiyo, itatuma kunakuwa mipango mpya za majibu na kufunguwa vituo vipya vya matunzo.


## CORONAVIRUS

### SWALI

Waliopona virusi ya corona wanafuatiliwa na chama (commission) gani ?

### JIBU

Kwa sasa, waliopona virusi ya corona wanafuatiliwa na vyama vya matunzo ya kisaikolojia, matunzo ya kinganga na upashaji wa habari za hatari na kazi ya kijamii, kulingana na hali. Vyama hivyo vinafuatilia waliopona kwa kuwaletea majibu ku magumu yenye inaweza watokea kuhusu kurudia ndani ya jamii, matokeo ya kisaikolojia pia na zingine magumu za afya kuhusu COVID-19.



Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio "Koma Ebola"

[soundcloud.com/user-740750674](https://soundcloud.com/user-740750674)  
[Facebook.com/komaebola](https://facebook.com/komaebola)  
[@Ebolakoma](https://twitter.com/Ebolakoma)  
[koma-ebola.info](https://koma-ebola.info)

## EBOLA

**SWALI**

Sababu gani vikundi vya waliopona vinagawanyika na japo vyote vinasema kama vanatumika kwa ajili ya wale watu waliopona ?

**JIBU**

Hakuna vikundi mingi inchini ya waliopona Ebola. Kikundi moja yenyi iko, inawasiliana na mpango wa ufuatiliaji ya waliopona Ebola kwa kuwasindikiza na kuwatunza. Lakini, kwa namna ya kusaidiana ndani ya kikundi, waliopona wenyi wanaishi mungini moja, commune moya... wanaweza kusanyika ndani ya vikundi ya kusaidiana. vile vikundi havi chukuwe fasi ya kikundi inchini ya waliopona.

## CORONAVIRUS

**SWALI**

Sababu gani COVID-19 inakamata sana wazee kuliko vijana ?

**JIBU**

Inafaa kujuwa kama mtu yeyote na wa myaka yoyote anaweza pata virusi ya corona. Ufundi imeonesha kama hata watoto wanaweza ambukizwa na hiyo virusi. Lakini ni ku sehemu ya ukingo mwilini njo inaonekana kama vijana wana resister kwa ile virusi zaidi kushinda watu wenyi wamesha kuwa na myaka mingi. Biyana biko na ukingo mwilini ya ku resister sana kwa kupiganisha magonjwa. Inaomba kujuwa pia kama wakati mtu anafikia ku myaka fulani, anakuwa katika hatari sana ya kupatwa na magonjwa ya nguvu, na mwili yake inapunguka nguvu sana. Ndio maana "hali ya myaka" ni ya lazima sana mu hali ya muripuko ya magonjwa sawa vile COVID-19.

Hii gazeti ina andikwa kwa msaada wa watu wa Amerika kupitia Shirika ya Amerika kwa maendeleo ya kimataifa (USAID). Yaliyomo haionyeshi maoni ya USAID na serikali ya Amerika.